



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kumb.Na.BA.1/25/01A/42

30 Juni, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi katika Ofisi ya Wakala wa Majengo Zanzibar kama ifuatavyo:-

1. Mhandisi Ujenzi Daraja la II – (ZPSG-08) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza katika fani ya Uhandisi Ujenzi (Civil Engineer) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

2. Mhandisi Mitambo Daraja la II – (ZPSG-08) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza katika fani ya Uhandisi Mitambo (Mechanical Engineer / Mechatronics Engineer) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Jinsi ya Kuomba:

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe **30 Juni, 2026** hadi tarehe **14 Julai, 2026**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini www.zanajira.go.tz.

- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanaJira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

KATIBU,

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,

S.L.P 1587,

ZANZIBAR

- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:

KATIBU,

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.

ZANZIBAR